ISSN 0856 - 034X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

***Supplement No. 21*** ***15th April, 2022***

***SUBSIDIARY LEGISLATION***

*To The Gazette Of The United Republic Of Tanzania No. 21 Vol. 103 Dated 15th April, 2022*
Printed By The Government Printer, Dodoma By Order Of Government

TANGAZO LA SERIKALI Na. 216 la tarehe 15/4/2022

SHERIA ZA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA),

(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Imetungwa chini ya kifungu cha 153)*

SHERIA NDOGO YA AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA YA HALMASHAURI YA WILAYA YA IKUNGI YA MWAKA 2022

Jina na Mwanzo wa Kutumika

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Afya na Usafi wa Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya Ikungi ya Mwaka 2021 na itaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Tafsiri

2. Katika Sheria Ndogo hii isipokuwa pale itakavyoelekezwa vinginevyo;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote atakayeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"chakula" maana yake ni kitu chochote kinacholiwa au kunywewa na binadamu isipokuwa dawa, hii ni pamoja na-

(a) kitu chochote kinachotumika katika matengenezo ya chakula;

(b) kitu chochote kinachoongeza ladha ya chakula; au

(c) kitu chochote kinachobadili rangi ya chakula;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi;

"kaya" maana yake ni familia inayojumuisha baba, mama, mtoto au watoto na mtu mwingine yeyote anayeishi na familia hiyo au watu wanaokaa katika nyumba moja na kuishi kama familia au mtu yeyote anayeishi peke yake katika chumba au nyumba;

"maji taka" maana yake ni kinyesi au mkojo na uchafu mwingine kama maji ya kuoga na maji ya kupigia deki, kuosha vyombo, maji yanayotokana na uchafu kutoka vituo vya mafuta, vituo vya kuoshea magari na viwandani ambapo yana kemikali au yasiyokuwa na kemikali na ambayo hayajasafishwa;

"mkazi" maana yake ni mtu yeyote anayeishi katika eneo la Halmashauri na ambaye ana kaya au anaishi katika kaya au taasisi iliyopo katika eneo la Halmashauri au anafanya biashara katika eneo la Halmashauri;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi au kikundi cha watu, kampuni, taasisi au shirika aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii.

Wajibu wa kufanya usafi wa mazingira

3.-(1) Kila mkazi anayemiliki eneo la nyumba, kiwanja au biashara atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kwamba anafanya usafi wa mazingira yanayozunguka makazi au eneo lake hadi mwanzo wa mipaka ya barabara ya mbele ya nyumba yake.

(2) Kila mmiliki wa nyumba, kiwanja au eneo la biashara atakuwa na wajibu wa kuondoa uchafu kama vile mchanga, majani, nyasi au vitu vingine vinavyofanana na hivyo kwenye mifereji ya kupitisha maji inayozunguka au kupita kando ya nyumba, kiwanja au eneo la biashara yake.

(3) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), na cha (2) kila mkazi atakuwa na wajibu wa kushiriki katika shughuli za usafi wa mazingira kila jumamosi ya mwisho

wa mwezi au katika siku itakayopangwa na Halmashauri.

(4) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kifungu atakuwa ametenda kosa.

Uwekaji taa za nje ya nyumba na upakaji rangi

4.-(1) Kila mmiliki wa nyumba au eneo la biashara atakuwa na wajibu wa kuweka taa yenye mwanga nje ya jengo analoishi au analolitumia kwa shughuli za biashara na atatakiwa kuiwasha wakati wa usiku.

(2) Mtu yeyote ambaye, bila sababu za msingi atakiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa.

Wajibu wa kuondoa na kudhibiti mazalia ya mbu

5.-(1) Mmiliki wa nyumba, kiwanja au eneo la biashara atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa katika eneo lake hakuna mkusanyiko wa maji, maji machafu, takataka au kitu chochote cha majimaji au kigumu ambacho kinaweza kuruhusu kuwepo kwa mazalia ya mbu au wadudu wengine wenye madhara kwa afya ya binadamu.

(2) Mtu yeyote ambaye bila sababu za msingi, atakiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa.

Upulizaji dawa

6.-(1) Mtu yeyote anayeendesha biashara ya upuliziaji dawa ya kuuwa wadudu au wanyama waharibifu katika eneo la Halmashauri atatakiwa:

(a) kuwa na cheti cha taaluma kinachotambuliwa na Serikali na leseni hai kutoka Halmashauri;
(b) kusimamiwa na Afisa Afya wakati wa upulizaji; na
(c) kutoa cheti baada ya kupuliza dawa kilichosainiwa na Afisa afya.

(2) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa.

Matengenezo na maegesho ya magari, pikipiki na mitambo

7.-(1) Matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo yatatakiwa kufanyika kwenye karakana, gereji au maeneo yaliyoruhusiwa baada ya kupata kibali rasmi kutoka Halmashauri.

(2) Mtu yeyote:

(a) hatoruhusiwa kutengeneza gari, pikipiki au mtambo wowote katika eneo la makazi, eneo la wazi au eneo ambalo halikutengwa kwa shughuli hiyo; au

(b) kuegesha gari bovu kwenye njia ya miguu, mtaa, uchochoro, mtaro, maeneo ya wazi au barabarani.

(3) Mtu yeyote atakayekiuka, bila sababu za msingi, masharti ya kifungu kidogo cha (2) atakuwa ametenda kosa.

Utengenezaji, na uuzaji vyakula.

8.-(1) Mtu yeyote anayetengeneza, kuchoma, kupika, kuchemsha au kuuza chakula cha aina yoyote katika eneo la Halmashauri atatakiwa:

(a) kutimiza masharti na kanuni za afya; na

(b) kuwa na kibali kutoka kwa Afisa Afya wa Halmashauri.

(2) Mtu yeyote atakayekiuka, bila sababu za msingi, masharti ya kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa.

Machinjio na maduka ya nyama

9.-(1) Mtu yeyote hatoruhusiwa:

(a) kwa madhumuni ya kibiashara kuchinja mifugo katika maeneo yasiyokuwa machinjio;

(b) kuuza nyama ya aina yoyote katika maeneo yasiyokuwa maduka ya nyama au katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri;

(c) kuuza nyama isiyokaguliwa na mtaalamu wa mifugo au mtaalamu wa afya; na

(d) kusafirisha nyama kwa madhumuni ya kibiashara kutoka machinjioni bila kutumia gari maalumu la kusafirishia nyama lililoidhinishwa na Halmashauri.

(2) Kila mmiliki wa duka la kuuzia nyama atatakiwa kuhakikisha yafuatayo:

(a) duka lake ni jengo la kudumu lililosakafiwa kwa marumaru nyeupe hadi urefu wa futi sita kutoka usawa wa sakafu;

(b) duka lake lina maji safi, misumeno ya kukatia nyama na vyuma vya kutundikia nyama;

(c) duka lake lina kabati la vioo na jokofu la

kuhifadhia nyama na mizani ya kupimia nyama;

(d) duka lake lina pipa au kifaa cha kuhifadhia takataka;

(e) muuzaji ana vazi jeupe pamoja na aproni nyeupe na kofia nyeupe;

(f) muuzaji anapima afya kila baada ya miezi sita; na

(g) duka lake lina karo la maji machafu.

(3) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) na (2) atakuwa ametenda kosa.

Uendeshaji wa biashara ya hoteli na hosteli

10.-(1) Kila mmiliki wa nyumba ya kulala wageni, hosteli, shule, kituo cha kutolea huduma za afya au nyumba ya biashara kabla ya kuanza biashara atakuwa na wajibu wa kuhakikisha:

(a) jengo lake limekaguliwa na Afisa Afya; na

(b) amepata kibali cha Halmashauri cha kufanya shughuli husika.

(2) Kibali cha kuendesha biashara ya nyumba ya kulala wageni, hosteli, shule, kituo cha kutolea huduma za afya au nyumba ya biashara kitatolewa baada ya Halmashauri kujiridhisha kuwa mahitaji yafuatayo yamezingatiwa: -

(a) jengo lina mwanga na hewa ya kutosha;

(b) jengo lina nafasi na vifaa vya kutosha;

(c) uimara wa jengo;

(d) jengo lina mfumo imara wa uondoshaji wa maji taka, miminika na taka ngumu;

(e) usafi wa jumla wa jengo na vifaa vyake;

(f) jengo lina vyoo na mabafu ya kutosha kwa jinsia zote;

(g) jengo lina vifaa vya zima moto;

(h) tanki la kuhifadhia maji safi;

(i) vyoo na bafu vimesakafiwa kwa vigae au marumaru na kuta zake zimewekwa vigae kiasi cha futi sita kutoka usawa wa sakafu;

(j) kwa nyumba za kulala wageni na hosteli, uwepo wa vyandarua.

(3) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kifungu cha (1) atakuwa ametenda kosa.

(4) Bila kuathiri masharti ya kifungu cha (3), wakati wowote Halmashauri ikijiridhisha kuwa mmiliki hajakidhi masharti ya afya inaweza kuzuia utoaji wa huduma husika mpaka hapo mmiliki atakapokuwa amekidhi masharti ya kiafya yaliyotolewa na Halmashauri.

Ukaguzi wa afya.

11. Halmashauri itatoza ada ya ukaguzi wa afya kabla ya kutoa au kuhuisha leseni ya biashara.

Eneo la kutupa taka

12.-(1) Halmashauri itakuwa na wajibu wa: -

(a) kutenga eneo maalum kwa ajili ya kutupia taka;
(b) kuweka vyombo maalum vya kutunzia taka katika maeneo ya Halmashauri; na
(c) kutoa huduma ya uzoaji taka kwa malipo kutoka kwa wazalishaji wa taka hadi kwenye dampo.

(2) Mtu yeyote atakayetupa taka au uchafu wowote au kuacha takataka au uchafu kwenye nyumba, uchochoro, kiwanja, mfereji wa maji ya mvua, barabara au mahali popote pasipotengwa kwa shughuli hiyo atakuwa ametenda kosa.

Vikundi vya wazoa taka

13. Halmashauri itahamasisha uundaji wa vikundi jamii na kuvitambua ili kuviwezesha kufanya shughuli za udhibiti wa taka ngumu pamoja na usafi wa mazingira katika mitaa baada ya kuingia mkataba na Halmashauri.

Magari ya abiria kuwa na vyombo vya kuhifadhia takataka

14.-(1) Kila mmiliki wa gari la abiria litakaloingia katika eneo la Halmashauri atatakiwa kuwa na chombo cha kuhifadhi taka na kuhakikisha kwamba kila abiria anatupa taka kwenye chombo hicho.

(2) Wamiliki wa magari ya abiria au madereva wao au makondakta watawajulisha abiria wao juu ya uwepo wa chombo cha kutupia taka katika magari yao ili abiria wasitupe taka kupitia madirishani.

(3) Endapo abiria atatupa takataka nje ya chombo cha usafiri, mmiliki au dereva au kondakta atachukuliwa kuwa ametenda kosa na atawajibika kulipa faini ya kiasi

kisichozidi shilingi elfu hamsini chini ya utaratibu wa kufifilisha kosa au kushtakiwa mahakamani chini ya Sheria Ndogo hii

Uhifadhi maji taka

15.-(1) Kila mmiliki wa nyumba, kiwanda au eneo la biashara anatakiwa-

(a) kuhakikisha kuwa analo karo la kuhifadhi maji taka;

(b) kunyonya maji taka pale karo linapojaa; na

(c) kutotiririsha au kutoelekeza maji kutoka vyooni, bafuni, karoni au viwandani kwenda barabarani, uchochoroni, mtoni, kwenye vyanzo vya maji, maeneo ya wazi, kwenye mfereji wa maji ya mvua au sehemu yoyote isiyotengwa kuhifadhia maji taka.

(2) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa.

Wajibu wa kuwa na choo na kukitumia

16. Kila mmiliki wa jengo la makazi au la biashara atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kwamba jengo lake lina choo safi, imara na madhubuti na kuhakikisha kuwa kinatumika wakati wote.

Vyoo vya umma

17. Halmashauri inaweza kujenga vyoo vya umma au kumruhusu mtu binafsi, vikundi vya watu au taasisi kujenga vyoo vya umma vitakavyotoa huduma kwa malipo katika maeneo ambayo Halmashauri itaona kuwa kuna haja ya kufanya hivyo.

Vyoo vya muda katika mkusanyiko

18.-(1) Mtu, kikundi au taasisi yenye lengo la kukutanisha watu kwa muda maalum katika eneo ambalo halina choo cha kudumu itatakiwa kujenga vyoo kwa matumizi ya wakati huo kwa idhini na usimamizi wa Halmashauri.

(2) Mtu, kikundi au taasisi itakayokiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) itakuwa imetenda kosa.

Ilani ya kujenga choo

19.-(1) Endapo katika ukaguzi wa afya itagundulika kuwa nyumba yoyote haina choo au choo kilichopo kimejaa au hakifai kwa matumizi ya binadamu, Afisa Mwidhiniwa atatoa ilani ya siku thelathini kwa mmiliki wa nyumba akiainisha masharti ya kurekebisha hali hiyo.

(2) Mmiliki wa nyumba atakayeshindwa kutekeleza masharti ya Ilani iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa.

(3) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1),

Halmashauri inaweza kuamuru nyumba au jengo hilo lisitumike kwa shughuli za makazi au
biashara hadi hapo hali hiyo itakaporekebishwa.

Ilani ya kuondoa kero

20.-(1) Endapo Afisa Mwidhiniwa atabaini kuwa eneo alilokagua lina kero yoyote atatoa ilani ya siku saba kwa mmiliki wa nyumba, mpangaji, mtumiaji au mtu yeyote anayehusika akimtaka kuondoa kero hiyo.

(2) Halmashauri inaweza kuamuru nyumba au jengo hilo lisitumike kwa makazi au biashara hadi hapo hali itakapokuwa imerekebishwa.

(3) Mtu yeyote atakayeshindwa kutekeleza masharti ya Ilani aliyopewa ndani ya muda ulioainishwa kwenye Ilani atakuwa ametenda kosa.

Upimaji wa afya

21.-(1) Kila mmiliki wa sehemu inayotoa huduma ya hoteli, mgahawa, baa, bucha, sehemu za kuokea mikate, nyumba za kulala wageni, grosari au mtu yeyote anayetengeneza chakula kwa ajili kuuza atatakiwa kuhakikisha kuwa wahudumu wake wanapima afya kila baada ya miezi sita.

(2) Mmiliki yeyote atakayekiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa.

Uteuzi wa wakala

22. Mkurugenzi anaweza kuteua kampuni,kikundi au mtu binafsi kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria Ndogo hii.

Adhabu

23. Mtu yeyote atakayetiwa hatiani kwa kosa lolote chini ya Sheria Ndogo hii atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote viwili kwa pamoja.

Kufifilisha kosa

24. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi laki mbili iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiyari na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoambatishwa katika Jedwali la Sheria Ndogo hii.

*Tangazo la Serikali Na. 216 (Linaendelea.)*

______

JEDWALI

________

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 24)*

________

HATI YA KUFIFILISHA KOSA

Mimi…………………………………………………….………. nakiri kwa hiari yangu mwenyewe mbele ya …………………………ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi/Afisa mwidhiniwa kwa niaba ya Mkurugenzi, kwamba Tarehe ………Mwezi………. Mwaka………. nilikutwa na kosa la kukiuka masharti ya Sheria Ndogo ya Afya na Usafi wa Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi ya Mwaka 2022, nipo tayari kulipa kiasi cha shilingi………………….na kutimiza wajibu wangu chini ya Sheria Ndogo hiyo badala ya kushtakiwa Mahakamani.

Nathibitisha kwamba maelezo hapo juu ni kweli na nimeyatoa kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu

Leo Tarehe………………………………. ya Mwezi…………………. Mwaka…………………

Jina………………………………………Saini………………………………………

Mbele ya:

Jina……………………………………...

Cheo…………………………………….

Saini………………………………………

Tarehe……………………………………

*Tangazo la Serikali Na. 216 (Linaendelea.)*

Nembo na muhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya IKUNGI umebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa Azimio lililopitishwa na mkutano wa Baraza la madiwani ulioitishwa Tarehe 22/1/2021 na ubandikwaji huo kushuhudiwa na:-

JUSTICE L. KIJAZI,
*Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya ,*
*Wilaya ya Ikungi*

ALLY J. MWANGA,
*Mwenyekiti Halmashauri ya*
*Wilaya ya IKUNGI*

**L.S**

NAKUBALI,

Dodoma,
9 Machi, 2022

UMMY A MWALIMU
*Waziri wa Nchi-OR-TAMISEMI*